SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

SHERIA NDOGO ZA (MATUMIZI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA ZA MWAKA, 2017

Jina

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Matumizi ya barabara) za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma za mwaka, 2017

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
.

Tarehe ya kuanza

3. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Tafsiri

4. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhinishwa**"** maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Gari**"** maana yake chombo chochote cha moto chenye kutumia magurudumu manne au zaidi.

"Barabara za Halmashauri" ni barabara zote ambazo zimejengwa na au zinamilikiwa na Halmashauri.

"Halmashauri**"** maana yake Halmashauri ya Manispaa ya Musoma;

"Kituo cha basi**"** maana yake kituo kilichotengwa mahususi kwa ajili ya kuegesha mabasi yanayoshusha na kupakia abiria;

“Kituo cha Teksi**”** maana yake tituo kilichosajiliwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha teksi;

“Lori**”** maana yake gari lolote lile la kubeba mizigo lenye uzito kuanzia tan 3 na kuendelea;

“Maegesho**”** maana yake sehemu iliyotengwa mahsusi na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha gari;

“Mkokoteni” maana yake chombo chochote chenye magurudumu kinachotumika kubeba mizigo ambacho hutembea kwa kusukumwa na binadamu au kukokotwa na mnyama, itajumuisha guta;

“Pikipiki na bajaji” maana yake ni chombo cha moto chenye magurudumu matatu kinachotumika kubeba abiria na mizigo.

“Mkurugenzi**”** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Mtaa**”** maana yake eneo lolote ndani ya Halmashauri na inajumuisha barabara;

“Teksi**”**maana yake gari yoyote iliyosajiliwa kwa madhumuni ya biashara na yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne;

“Wakala**”** maana yake mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo litakuwa limepewa mamlaka na Halmashauri ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri;

Maegesho

5. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari nje ya eneo lililotengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(2) Halmashauri kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola itaweka alama za barabarani za kuonyesha sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha magari katika mitaa yote ndani ya Halmashauri.

Usajiri wa Teksi

6. (1) Kila teksi itatakiwa kusajiliwa na Halmashauri kabla ya kuanza kufanya biashara ya kusafirisha abiria.
(2) Kabla ya teksi hiyo kusajiliwa, mmiliki atahakikisha kwamba gari lake limelipiwa kodi zote zinazotakiwa na serikali ikiwa ni pamoja na ada na ushuru wa Halmashauri.

(3) Niwajibu wa kila mmiliki wa teksi kuchora mstari wa njano ubavuni mwa teksi kabla ya teksi kukaguliwa na kusajiliwa.

(4) Baada ya teksi kusajiliwa, Halmashauri itatoa namba na kuainisha kituo ambacho teksi iliyosajiliwa itaegeshwa.

(5) Kila usajili wa teksi utadumu kwa muda wa mwaka mmoja, baada ya hapo mmiliki wa teksi atawajibika kuhuisha usajili wa teksi yake.

(6) Mtu yeyote ambaye hatahuisha usajili wa teksi kwa wakati atawajibika kulipa gharama za usajili pamoja na tozo la shilingi hamsini elfu (50,000/=) kama adhabu.

7. (1) Halmashauri itatenga, kusajili na kutangaza maeneo rasmi kwa ajili ya kutumika kama vituo vya teksi .

(2) Halmashauri itabainisha idadi ya teksi zitakazoruhusiwa kuegeshwa katika kituo kimoja kwa wakati mmoja kwa kuzingatia ukubwa wa eneo husika.

8. (1) Nimarufuku kwa lori lenye uzito wa tani $7^1/_2$ kuingia maeneo ya barabara za mjini kati bila kupata kibali cha maandishi cha Halmashauri.

(2) Kibali cha kuingiza lori katika maeneo ya barabara za mjini kati kitalipiwa ada ya shilingi 100,000/= kwa kila safari ya kuingia.

(3) Kibali kilichotolewa kitatumika kwa safari moja kwa siku moja kwa muda uliotajwa kwenye kibali na kwa barabara zitakazoainishwa ndani ya kibali hicho.

Kuosha magari sehemu zisizoruhusiwa

9. (1) Nimarufuku kwa mtu yeyote kuosha gari katika eneo la barabara, hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo halikutengwa kwa matumizi ya kuosha magari.

(2) Gari ambalo litakutwa likioshwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), litavutwa na kuhifadhiwa mahali ambapo Halmashauri itaona panafaa na mmiliki wa gari hilo atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja.

(3) Mmiliki wa gari iliyovutwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa, pamoja na faini iliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2), kulipa shilingi elfu hamsini ambazo ni gharama za kuvuta gari na shilingi elfu kumi na tano kwa siku kama gharama ya kuhifadhi gari(4) Iwapo gari lililovutwa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi litakaa bila kuchukuliwa kwa muda wa siku thelathini na mmiliki wake, Halmashauri italiuza gari hilo kwa mnada ili kufidia gharama zake na kiasi cha fedha kitakachobaki atarudishiwa mmiliki wa gari husika.

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote kufunga barabara kwa ajili ya sherehe, msiba au shughuli nyingine yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri. Ufungaji wa barabara

11. Ni marufuku kwa mtu yeyote yule kuweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kama kokoto, mchanga, mawe, mbao na vifaa vinginevyo vya ujenzi kwenye barabara, hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhusiwa bila ya idhini ya maandishi ya Halmashauri. Uwekaji wa vifaa vya ujenzi barabaranii

12. (1) Nimarufuku kwa mtu yeyote kukata barabara kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji, nyaya za umeme, simu au shughuli nyingine yoyote ile bila ya kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

(2) Kibali cha kukata barabara kitadumu kwa muda wa siku saba na baada ya hapo endapo muombaji atashindwa kurekebisha eneo lililokatwa na kurejesha barabara katika hali ya awali atatozwa faini pamoja na kurekebisha kwa kiwango cha awali. Kukata barabara

(3) Ni marufuku kwa aina yeyote ya mifugo kuonekana inazuiliwa katika barabara

13. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo:-

a) Ataegesha gari katika sehemu isiyoruhusiwa;

b) Atafanya biashara ya teksi kwa kutumia gari ambalo halijasajiliwa au ataegesha teksi kwenye eneo ambalo sio kituo cha teksi
c) Ataendesha mkokoteni ambao haujasajiliwa;

d) Ataendesha mkokoteni katika barabara ambayo haijaruhusiwa;

e) Ataosha gari katika eneo la barabara, hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo matumizi yake siyo ya kuoshea magari;

f) Atafunga barabara kwa shughuli za sherehe, msiba au shughuli nyingine yoyote bila kibali cha Halmashauri;

g) Atakata barabara bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri;
Ataweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kwenye barabara, hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhusiwa;

h) Atapitisha wanyama, ng'ombe, mbuzi, kondoo, kwenye barabara;

i) Atamzuia Afisa au Wakala wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi;
j) Atakaye haribu miundombinu.
k) Ataweka matuta kihorela

(2) Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi atatozwa faini ya shilingi za kitanzania kiasi kisichopungua shilingi za kitanzania laki mbili na kisichozidi shilingi za kitanzania milioni moja elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili jela au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Makosa na adhabu

14. Mfugo wowote utakaokutwa unapita katika barabara utakamatwa na kuhifadhiwa katika yadi ya Halmashauri na mwenye mifugo atalipia gharama za utunzaji kwa kila mfugo kiasi cha shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) kwa siku kwa mfugo mmoja.

15. (1) Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili na isiyozidi milioni moja mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri.

JEDWALI LA KWANZA

ADA YA KIBALI CHA KUKATA BARABARA

i. Tshs 500,000/=……kwa barabara za lami
ii. Tshs 250,000/= …….. kwa barabara za changarawe
iii. Tshs 100,000/= ……...kwa barabara ya vumbi

JEDWALI LA PILI

ADA YA KIBALI CHA KUFUNGA BARABARA

1. Kufunga barabara kwa saa chini ya saa 1 …….. tshs 50,000/=
2. Kufunga barabara kwa masaa 1 – 3..... ……..tshs 100,000/=
3. Kufunga barabara kwa masaa 3 – 6 ..... ……tshs .200,000/=
4. Kufunga barabara kwa masaa 6 – 12..... ……tshs 500,000/=

5. Kufunga barabara kwa masaa 24 ..... ……tshs 1,000,000

JEDWALI LA TATU

MAOMBI YA KIBALI CHA KUKATA/ KUFUNGA BARABARA

1. Jina la mwombaji …….
2. Anwani/ Namba ya simu ya mwombaji ……..
3. Maombi ya …….
4. Barabara itakayohusika ……
5. Muda unaoombwa kwa ajili ya kukata/ kufunga barabara ……..
6. Saini ya Mwombaji ……
7. Tarehe ……
   MAONI YA UONGOZI WA MTAA ENEO BARABARA ILIPO

   ……
   ……
   ……...

(KIBALI)

KIBALI CHA KUKATA/ KUFUNGA BARABARA

1. Jina la mwombaji ……..
2. Anwani/ namba ya simu ya mwombaji ……
3. Maombi ya …… barabara
4. Barabara itakayohusika ……
5. Muda wa kibali ni kuanzia tarehe ……. hadi tarehe ……
6. Masharti ya kutumia kibali hicho

   (a) ……...

   (b) ……

   (c) ……

   (d) ……

   (e) ……
7. Imesainiwa na

   Jina …….

   Saini …… ……

   Afisa wa Halmashauri ya Manispaa

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi ufuatia Azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa kilichofanyika tarehe …… mwezi …… 2017 mbele ya:

……..
MH. PATRICK GUMBO
MSTAHIKI MEYA
MANISPAA YA MUSOMA

……
FIDELICA G MYOVELLA
MKURUGENZI
MANISPAA YA MUSOMA

NAKUBALI,

……
TAREHE ……. MH. **GEORGE B. SIMBA CHAWENE (Mb)**
DODOMA **WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI**